# MWONGOZO WA MOAMBI: MASWALI YA UKAGUZI WA AWALI WA UVUMBUZI

OKTOBA 5, 2020

CREATING HOPE IN CONFLICT: A HUMANITARIAN GRAND CHALLENGE

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Ministry of Foreign Affairs of the Netherlands

WITH SUPPORT FROM Grand Challenges Canada® Grands Défis Canada

Photo Credit: GETTY IMAGES / ICRC / OU, Ed. 2011, Makhmour, ICRC-supported primary health-care centre. Laboratory personnel at work. V-P-IQ-E-01080

## MWONGOZO WA MOAMBI: MASWALI YA UKAGUZI WA AWALI WA UVUMBUZI

- Mwongozo huu wa maombi unaambatana na Ombi la pili la Pendekezo la Mradi chini ya Kutengeneza Tumaini katika Machafuko: Changamoto Kubwa za Kibinadamu
- Mwongozo huu wa maombi umeandaliwa ili kuwasaidia wavumbuzi watarajiwa (k.m. waombaji) kuwasilisha maombi yenye tija.
- Maombi yote yaliyokamilika na yenye sifa yanapitia mchakato wa mapitio wa hatua mbalimbali, ikiwemo mapitio ya ndani na ya nje.
- Hatua ya kwanza kwenye mchakato wa maombi ni ‘Ukaguzi wa Awali wa Uvumbuzi’.

Waombaji wanapaswa pia kupitia nyaraka zifuatazo za msingi kabla ya kuwasilisha maombi:

- Ombi la Pendekezo la Mradi, Kutengeneza Tumaini katika Machafuko: Changamoto Kubwa za Kibinadamu
- Changamoto Kubwa za Kibinadamu: Uchambuzi wa Vizuizi

Zinapatikana kupitia https://humanitariangrandchallenge.org/

# MUHTASARI WA 'UKAGUZI WA AWALI WA UVUMBUZI'

Zingatia: Mnamo 2018 takribani asilimia 55 ya maombi yalishindwa kufaulu Ukaguzi wa Awali wa Uvumbuzi.

Dhumuni la Ukaguzi wa Awali wa Uvumbuzi ni kufanya uhakiki wa haraka wa maombi yote, ili kuchagua yale yatakayopitiwa kwa kina zaidi.

- Wahakiki wanaangalia tu maswali manne ya kwanza ya maombi kwa ajili ya vumbuzi za Seed na maswali matano ya kwanza kwa vumbuzi za Transition-toscale.
- Wahakiki hao ni mchanganyiko wa wafanyakazi wa Grand Challenges Canada (GCC) na wafanyakazi wa mashirika ambayo ni wabia wa GCC.
- Wahakiki wanatoka katika taaluma mbalimbali, baadhi wakiwa na uzoefu mkubwa katika sekta ya kibinadamu, na wengine wakiwa na uzoefu mdogo wa kibinadamu lakini ni wataalamu wa mambo mengine.
- Ili kuongeza nafasi ya kufanikiwa, maombi yanapaswa kutoa majibu ya moja kwa moja na ya wazi kwa kila swali.
- Kurasa zifuatazo zinatoa mifano ili kuwaongoza wavumbuzi katika kuandaa maombi yao. Mifano iliyotolewa kwenye mwongozo huu inatokana na maombi yaliyopokelewa mwaka 2018.

# Swali #1: Je, ni tatizo gani linashughulikiwa na uvumbuzi wako? (kikomo cha herufi 500)

Mwongozo: Wavumbuzi wanapaswa kuweka mkazo katika kulielezea tatizo mahsusi ambalo uvumbuzi wako unalitatua. Chukulia kwamba mpitiaji hana uelewa kabisa kuhusu muktadha au tatizo husika. Hitimisha na namna uvumbuzi wako unavyolitatua tatizo hili kwa kutumia sentensi moja. Swali linalofuata (Swali #2) litakuwezesha kuuelezea uvumbuzi wako kwa kina zaidi.

Makosa ya kawaida:

• Tatizo linaloshughulikiwa ni la kiujumla/kubwa sana (k.m. "masuala ya mazingira na ya kijamii")
• Uvumbuzi unaopendekezwa si sahihi kwa tatizo ambalo linashughulikiwa
• Hakuna maelezo yaliyotolewa kwa tatizo lililotambuliwa (k.m. "kuzuia magonjwa")
• Kuelezea tatizo husika kwa kutumia maneno ya kifalsafa (k.m "shughuli za kibinadamu zinasababisha kutokea janga la kidunia")
• Majibu yanayohusisha takwimu peke yake. Ingawa takwimu zinaweza kuwa na tija, majibu yanapaswa pia kutoa maelezo na kuwianisha takwimu husika na uvumbuzi wao.

| Mfano Mbaya | Mfano Mzuri |
|---|---|
| "1.Kuzuia magonjwa kwa njia ya FREE-ORGAN-SCAN-SCREENING<br>2.Shughuli/programu za utafiti kuhusu visababishi vya ongezeko la vifo katika nchi zilizo chini ya jangwa la Sahara-Afrika<br>3. Uzalishaji wa dawa za asili zenye ubora, ufanisi na unafuu.<br>4. Kudhibiti ongezeko la milipuko ya kipindupindu kwa kutengeneza sabuni, sabuni za kusafishia na viuaviini zenye ubora, ufanisi na unafuu." | "Uvumbuzi XYZ unashughulikia matatizo matatu yanayotokea wakati wa upasuaji kwenye maeneo ya machafuko na majanga ya kibinadamu. 1) Usalama wa wagonjwa – hatari kubwa za maambukizi kwenye vituo visivyosafishwa vizuri ili kuua viini. 2) Usalama wa watoa huduma – hatari za maambukizi zinazidishwa na uhafifu wa vifaa vya kujikinga, kama ilivyobainishwa lakini haikomei tu katika janga la Ebola. 3) Uwezo wa upasuaji – vituo ni sehemu zinazolengwa na mashambulizi na wanatimu wanapaswa kuwa wepesi, na hivyo kupunguza alama ya miundombinu na kurahisisha minyororo ya ugavi ni jambo muhimu." |
| "Wilaya ya Kibondo imekuwa ikihifadhi wakimbizi kwa takribani muongo mmoja sasa, ambao kwa sehemu kubwa wanatokea nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Burundi. Kwa sasa tuna kambi ya Nduta inayohudumia wakimbizi 150,000 kutoka Congo na Burundi. Uwepo wa wakimbizi umeleta madhara kwa mazingira, mwingiliano wa kijamii, usalama na milipuko ya mara kwa mara ya magonjwa katika vijiji vinavyopakana na kambi. Jumuiya inayoihifadhi kambi hii haina huduma za kijamii ikiwemo ugavi wa maji" | "Mnamo mwaka 2017 idadi ya kesi za rotavirus duaniani iliongezeka pale zaidi ya watu milioni 1 walipoambukizwa katika Yemeni iliyokumbwa na vita. Mikakati ya kukinga magonjwa si vipaumbele kwenye maeneo yaliyokumbwa na vita, kutokana na jitihada zinazohitajika kulingana na mbinu za hivi sasa za ubainifu. Kadhalika, mashirika ya misaada yanafanya kazi kwa saa nyingi ili kuzuia magonjwa kusambaa. Kubaini mapema viini vya rotavirus kwenye maji kwa kutumia kifaa kinachotoa majibu ya haraka na kinachobebeka kunaweza kuwezesha mikakati makini ya uponyaji." |
| "Kazi kubwa ya kibinadamu kwenye sayari hii inaendeshwa na kuchochewa na mfumo wa kupewa tuzo ya kifedha, mfumo huu wa kurithi unafanya kazi kama aina ya utumwa wa kiuchumi. Udhalimu wa kifedha uliosababishwa na mfumo huu huwalazimisha wanadamu kufanya kile wanachohitaji kufanya, ili kutengeneza kipato cha fedha kitakachowafanya waendelee kuishi. Matokeo ya shughuli hii ya kibinadamu inapelekea janga la kidunia. Jambo linalotia wasiwasi sana, utambuzi wa janga hili la kidunia kwa sasa ni dhahiri, lakini hakuna suluhisho zilizopo ili kulitatua tatizo hili." | "Uvumbuzi wetu unashughulikia janga la kidunia la kupika chakula pamoja na mahitaji husika ya nishati ya joto kama upashaji joto wa eneo na kuua viini kwenye maji. Wale wanaoishi kwenye kanda zenye machafuko mara nyingi ni kati ya watu wenye uhitaji wa nishati. Katika hali za dhiki kama hizo, karibia kila dutu iwakayo inaweza kutumika kama kitu cha kuwashia moto, hata kama ni hatari, kinatoa hewa yenye madhara, au hupelekea ukataji haramu wa miti. Uvumbuzi XYZ ni jukwaa la nishati linalozalisha nishati mbadala ya bure kwa namna ambayo ni salama na isiyotoa hewa chafu." |

# Swali #2: Je, uvumbuzi wako unaopendekezwa ni upi? (kikomo cha herufi 500).

Mwongozo: Wavumbuzi wanapaswa kuweka mkazo katika kuuelezea uvumbuzi wao kwa kutumia lugha rahisi ya Kiingereza au Kifaranasa, wakiepuka kutumia vifupisho au lugha ya kitaalamu. Jibu lako kwa swali hili linapaswa kuwianisha waziwazi tatizo husika dhidi ya swali lililopita. Majibu yanapaswa kuelezea waziwazi kitu gani ni kipya/tofauti kuhusu wazo lako, na kwa namna gani vipengele hivi vya kivumbuzi vinatatua tatizo lililotambuliwa katika Swali #1.

Makosa ya kawaida:
• Miradi inayopendekezwa inayopanga kutumia utafiti kama lengo kuu
• Jibu linaelezea nini kitafanyika, lakini si ule uvumbuzi halisi unaopendekezwa (k.m. kuboresha ugavi wa maji kwa njia ya uchimbaji wa visima)
• Jibu linajumuisha vijenzi mbalimbali, bila ya kuwa na vitu vipya/vya kivumbuzi (k.m. uchimbaji wa visima na kuelimisha jamii)
• Linajumuisha lakini linashindwa kuelezea waziwazi vijenzi vikuu vya uvumbuzi husika (k.m. kuwianisha sarafu ya kidijitali, blockchain, upumuaji na uwezeshwaji kiuchumi katika uvumbuzi mmoja)

| Mfano Mbaya | Mfano Mzuri |
| --- | --- |
| “Kuendeleza maono 2030 kwa kutumia mbinu ya kuzuia magonjwa ni bora kuliko tiba kwa watu maskini wenye kipato cha chini ambao kipato chao ni chini ya dola 2 kwa siku, yaani hawawezi kununua dawa. Programu za utafiti zinazolenga kupunguza ongezeko la kiwango cha vifo kwenye maeneo ya vijijini ya Kenya na Tanzania ambapo wagonjwa maskini hawamudu gharama kubwa za huduma za afya. Kudhibiti ongezeko la milipuko ya kipindupindu kupitia ununuzi wa malighafi, uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa sabuni n.k.” | “Uvumbuzi XYZ unatafakari upya suala la upasuaji salama kwa kutoa a mkazo wa kinga kutoka vyumba vya upasuaji kwenda mkato wenyewe. Ni kitambaa kilicho wazi na safi ambacho:<br>- kinajazwa hewa safi katika ugo ulio juu ya mkato<br>- kinafikiwa na watoa huduma kupitia mkono na nyenzo za vifaa<br>- kinashikilia kisinia cha upasuaji ndani yake<br>- kinatosha kwenye begi la mgongoni au eneo kama hilo kama kifaa kilicho tayari kutumika haraka<br>- kinaweza kuandaliwa kwa haraka kupitia mifumo iliyopo ya upasuaji” |
| “Kuboresha ugavi wa maji kwenye vijiji 11 karibu na Kambi ya Wakimbizi ya Nduta, kuanzisha kampeni ya elimu ya afya kwa jumuiya kuhusu utupaji sahihi wa taka ngumu na maji taka kutoka majumbani mwao kwa Kuendesha utafiti wa maji ya ardhini, Kuchimba visima na kufunga pampu za maji zinazotumia nishati ya jua, Kujenga lambo la maji, Kuanzisha laini za usambazaji na vituo vya ukusanyaji na Uundaji wa vyombo mahalia vitakavyoongeza uendelevu wa mradi.” | “Tumeunda kifaa cha uchunguzi kinachotumia simu ya kisasa ambacho kinakuza DNA ili kubaini kipindupindu, chanzoni, chini ya dakika 30. Data husika inapakiwa papo hapo kwenye seva inayotumia teknolojia ya “cloud” ili kuendesha mchakato wa uingizaji wa data. Kwenye maeneo yasiyo na intaneti, kiungio cha Wifi kinaweza kutumika kwenye eneo kuu kwa ajili ya upakiaji wa data. Uvumbuzi XYZ ni kifaa cha kwanza na pekee kinachobaini kipindupindu kwa kutumia maji huku kikiendesha mchakato wa uingizaji data kwa kualamisha muda mahsusi na taarifa ya eneo la kijiografia” |
| “Mradi XYZ unatokana na mfumo wa kimapinduzi wa kutoa tuzo kwa ajili ya mazoezi ya Kupumua, Tafakuri na Yoga kwa kutumia Teknolojia ya Blockchain. Mradi wa XYZ ni wa kwanza wa aina yake katika Sekta ya FinTech ya Huduma ya Afya inayoweka mkazo kwenye Kukinga Magonjwa. Mfumo huu mpya, unatoa tuzo kwa mazoezi ya muda mrefu ya kupumua, tafakuri na yoga, shughuli zote zikiwa na manufaa ya kiafya yaliyothibitishwa kisayansi. Lengo kuu la mradi huu ni kuwapa tuzo watendaji kwa kutumia sarafu ya kidijitali, tunayotumaini itakuwa na thamani kuliko kima cha chini” | “Uvumbuzi XYZ unakusanya, unahifadhi na unaokoa nishati ya jua kwenye mikebe inayobebeka. Watumiaji wanaweza kupika mahali popote na wakati wowote kwa kutumia nishati ya bure ya jua, hata ndani na wakati wa usiku. Uvumbuzi XYZ unaweza kutumika kupasha joto eneo fulani, kuua viini kwenye maji kwa kutumia joto. Tunafanyia kazi kifaa cha kuongeza umahiri wa uvumbuzi mama kwa ajili ya uhifadhi wa muda mrefu, wakati wa msimu wa mvua. Kazi yoyote inayohitaji nishati iliyohifadhiwa na inayobebeka kutoka chanzo mbadala inaweza kutekelezwa kwa uvumbuzi wa Uvumbuzi XYZ.” |

# Swali #3: Je, zipo hatua gani hivi sasa zinazotatua tatizo husika na kwa namna gani uvumbuzi wako unaweza kulishughulikia kwa ufanisi zaidi? (kikomo cha herufi 500).

Mwongozo: Waombaji wanapaswa kutaja mbinu mbadala zilizopo hivi sasa za kushughulikia tatizo wanalolitatua. Majibu yanapaswa kubainisha ni vitu/vipengele/vijenzi gani vya uvumbuzi wako ni bora kuliko suluhisho zilizopo kwa sasa.

Makosa ya kawaida:

- Kushindwa kuelezea hatua gani za hivi sasa/awali zinazoshughulikia tatizo husika, na kwa nini hatua hizo zinashindwa kuleta matokeo
- Maelezo ya hatua za hivi sasa ni mapana sana/ya kifalsafa (k.m. kubadilisha mifumo ya sasa ya kiuchumi)
- Majibu yanashindwa kuelezea waziwazi ile thamani inayoongezwa na uvumbuzi unaopendekezwa. Kwa mfano: Je, uvumbuzi wako utaboresha spidi, ubora, na/au gharama ya bidhaa au huduma fulani? Kama ni hivyo, namna gani?

| Mfano Mbaya | Mfano Mzuri |
| --- | --- |
| "Kutokana na umaskini, huduma za bure za upimaji zitawavutia watu wengi mahalia ambao ni maskini kupitia kliniki zinazohamishika zilizo nadhifu/zinazoratibishwa kwa kushirikiana na wadau husika. Usambazaji wa sabuni, sabuni za kusafishia na viuaviini utawavutia maskini wengi wahitaji ambao kipato chao ni chini ya dola 2 kwa siku. Kufanya utafiti kuhusu dawa za kiasili ni suluhisho bora kwa kizazi hiki cha usugu wa dawa. Zaidi ya asilimia 80 wanatumia dawa za asili hapa Afrika – kujumuisha Kenya na Tanzania. | "Usalama wa wagonjwa: suluhisho za hivi sasa zinapakia vyumba na mifumo ya upitishaji hewa kwenye mahema, malori, n.k. Uvumbuzi wetu unatoa kinga ya kisasa, hautegemei umeme/halinchi/barabara, una gharama nafuu, na matengenezo kidogo. Usalama wa watoa huduma: tofauti na nguo na vitambaa vya upasuaji, Uvumbuzi XYZ unazuia kikamilifu maambukizi ya wagonjwa, bila ya wanatimu kuvaa vifaa vizito na vianvyoleta joto. Kikiwa kama kifaa kimoja, kinarahisisha pia minyororo ya ugavi. Uwezo wa kufanya upasuaji: Uvumbuzi XYZ unaacha alama ndogo sana na unaweza kwenda popote ambapo mtoa huduma anaweza kwenda" |
| "Mradi huu utajumuisha mbinu ya ubia. Mradi huu utaanza kwa tathmini shirikishi ya miradi ya hivi sasa ya usafi kwenye jumuiya na mashule yaliyopo kwenye vijiji husika ambapo Tawala za Wilaya zitahusishwa kikamilifu wakati wa mchakato wa utambuzi wa vizuizi mahalia, hatari kuu na taratibu zinazohitaji maboresho. Matokeo, mahitimisho na mapendekezo ya tathmini hizi, yatawezesha wabia husika kuweka mipango na kufanya utekelezaji wa pamoja" | "Uvumbuzi XYZ ni kifaa kwa kwanza na pekee cha kuchunguza kipindupindu kwa kutumia maji na cha kwanza cha aina yake kuendesha mchakato wa uingizaji data kwa kualamisha muda na taarifa ya eneo la kijiografia. Jukwaa hili litawezesha hatua za mapema, badala ya za kimwitikio katika ubainifu wa viini vya kwenye mazingira." |
| "Mradi huu ni wa kwanza wa aina yake. Hatimaye mfumo wa XYZ unalenga kubadilisha uchumi wa Keynesian na kuwa uchumi wa Buddha afanyaye shughuli za Kibinadamu. Jambo hili linawezesha uendelevu binafsi wa kifedha kwa kufanya mazoezi yaliyothibitishwa kisayansi kama vile yoga na tafakuri." | "Majaribio yaliyopita ya kupika kwa kutumia nishati ya jua yanahitaji mtu apike nje kwenye jua wakati wa mchana, na mara nyingi kwa kutumia joto la kiasi cha chini, sawa na jiko la moto mdogo. Kupika wakati wa mchana kunaweza kuwaweka watumiaji kwenye hali hatarishi katika maeneo yaliyokumbwa na vita. Teknolojia za hivi sasa za nishati ya jua zinaweza pia kutoheshimu tamaduni na desturi za upikaji kwa kuhitaji watu kupika kwenye kasha, chungu maalum, au bomba. Kwa Uvumbuzi XYZ, mtumiaji anaweza kupika jinsi apendavyo, kwa kutumia chungu au kikaangio chochote, na wakati ambao ni salama kabisa, ikiwemo usiku." |

# Swali #4: Elezea jinsi uvumbuzi wako ulivyo na manufaa kwa watu walio kwenye mazingira hatarishi, yasiyofikika kwa urahisi walioathiriwa na migogoro? (kikomo cha herufi 500).

Mwongozo: Waombaji hawapaswi kuweka mkazo katika kufasili mara ya pili tatizo husika ambalo tayari limeshafasiliwa katika Swali #1. Kwanza kabisa majibu yanapaswa kuelezea wanaolengwa na vumbuzi zao ni kina nani, na kuelezea namna na kwa nini uvumbuzi husika una manufaa kwa walengwa (k.m. jumuiya zilizoathiriwa na machafuko). Majibu yanapaswa kuelezea namna uvumbuzi husika unavyofahamu mahitaji ya walengwa na ni kwa namna gani walengwa hao wataufikia/watautumia uvumbuzi unaopendekezwa.

Makosa ya kawaida:

- Kuyarejelea maeneo yasiyo na migogoro (k.m. "katika sehemu nyingi za Afrika")
- Majibu hayaweki mkazo katika mgogoro, bali yanaongelea masuala mengine ya kijamii (k.m. "umaskini na utumwa wa kiuchumi")
- Majibu yanashindwa kuelezea namna walengwa watakavyoufikia au watakavyoutumia uvumbuzi husika (Je, walengwa watautumia moja kwa moja? Au Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi kwenye machafuko yatautumia uvumbuzi husika ili kuwahudumia walengwa?)

| Mfano Mbaya | Mfano Mzuri |
|---|---|
| "Katika maeneo mengi ya Afrika, maskini wanakaa vijijini ambapo hakuna huduma za maji safi ya kunywa wala umeme. HOSPITALI za serikali wakati mwingine zinajengwa kilomita kadhaa mbali hivyo usafiri ni mgumu sana kwa kuwa barabara ni za udongo au tope. Hivyo KILINIKI ZINAZOHAMISHIKA ambazo mimi nazipendekeza zitaratibiwa kuwepo kwenye mazingira ya kijijini ili kuhudumia moja kwa moja mifumo duni ya ikolojia zinaweza kupeleka huduma ya afya kwa wahitaji kupitia mbinu ya nyumba kwa nyumba." | "Uvumbuzi XYZ ni nafuu, unabebeka kwa urahisi, ni rahisi kuutumia, na unaacha alama ndogo sana, unatoa mahitaji makubwa ya huduma ya upasuaji kwa watu wasiofikika kwa urahisi ambao ameathitiriwa na machafuko au majanga ya asili. Umesadifishwa na kupimwa kwa ajili ya upasuaji wa maumivu zaidi, wa kawaida na wa ob/gyn ambao ni muhimu kwa watu hawa, kulingana na uzoefu wa wanatimu wanaofanya kazi huko Afganistan, Iraq, Syria na nchi nyinginezo." |
| "Kwa kuboresha ugavi wa maji jumuiya husika itapata ufikio endelevu wa maji safi ya kunywa na usafi wa mazingira hivyo kuchangia katika kuboresha hali za maisha za vikundi vilivyo kwenye mazingira hatarishi. Maji na usafi ni mambo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kibinadamu na mifumo thabiti ya ikolojia. Kwa ongezeko kubwa la watu na mabadiliko ya tabia nchi, shinikizo kwenye vyanzo vya maji safi limeongezeka kwa sehemu kubwa, na kuongeza ushindani kati ya watumiaji wake." | "Uvumbuzi XYZ ni kifaa cha uchunguzi kinachotumia simu ya kisasa ambacho kimeundwa kwa ajili ya kutumiwa kwenye chanzo cha mazingira na wafanyakazi wa uwandani. Upimaji mwingi wa uchunguzi wa dunia unafanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; hivyo basi, teknolojia ya kivumbuzi ya Uvumbuzi XYZ itashughulikia nyanja nyingi ngumu zinazohusika kubaini viini kwa watu walio kwenye mazingira hatarishi wanaokabiliwa na machafuko. Faida kuu ni kwamba kifaa hiki kinaondoa hitaji la mnyororo wa uhifadhi wa baridi. Jambo hili linafanya kusafiri kwenye maeneo yenye migogoro kuwa rahisi kwa sababu ya uendeshaji mwepesi." |
| Umaskini uliokithiri na ukosefu wa usawa ni tatizo kubwa zaidi la pili duniani, ambapo la kwanza ni mfumo wa utumwa wa kiuchumi. Kipaumbele cha mradi huu ni kulenga/kutuza watu walioathiriwa na umaskini ambao wapo kwenye maeneo ya machafuko, kwa kuwatuza kifedha kwa kutumia sarafu ya kidijitali. Jambo hili litawawezesha kiuchumi watu hao na kuwasaidia katika kuendeleza maisha yao." | "Uvumbuzi XYZ hauhitaji kitu cha kuwasha moto, kama kuni, mkaa, au bidhaa zinazotokana na petroli ambazo zinaweza kutopatikana kwa watu wasiofikika kwa urahisi wanaoathiriwa na machafuko. Mionzi ya jua tu ndiyo inayohitajika kuendesha Uvumbuzi XYZ." |